



TANZANIA CHAMBER OF COMMERCE, INDUSTRY AND AGRICULTURE

P. O. Box 9713 Dar es Salaam, Tanzania Tel: 255 – 22 – 2119437 Fax: 255 – 22 – 2119436

Email: hq@tccia.com , info@tccia.com , Web site: <http://www.tccia.or.tz>

6 Octoba 2023

TAARIFA

TANGAZO LA UCHAGUZI WA TCCIA NGAZI YA TAIFA

Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) inapenda kuwatangazia wanachama wake kuwa uchaguzi wa kujaza nafasi za uongozi ngazi ya Makao Makuu utafanyika tarehe 07/11/2023 kwa mujibu wa katiba ya chemba na kufuata kanuni zake kama zinavyoelekeza, yaani “ **Regulations Made Under Tccia Memarts And Its Amendments 2017**” kama zilivyoambatanishwa.

Nafasi zilizo wazi ni kama ifuatavyo:

- I. Rais wa TCCIA
- II. Makamu wa rais wa TCCIA-Biashara
- III. Makamu wa rais wa TCCIA-Viwanda
- IV. Makamu wa rais wa TCCIA-Kilimo

Kila mgombea anatakiwa kutimiza masharti yafuatayo:

- I. Kujaza fomu ya kugombea uongozi (nomination form) na kuiwasilisha makao makuu ya TCCIA.
- II. Masharti mengine Kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi za TCCIA mwombaji anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:
 1. Mfanyabiashara mahiri.

2. Kuwasilisha hesabu za fedha zilizokaguliwa za kampuni au biashara kwa miaka miwili iliyopita.
3. Ushahidi wa kufuata sheria na kanuni za biashara
4. Ushahidi wa malipo ya ada ya uanachama kwa miaka miwili iliyopita na haipaswi kuwa na malimbikizo yoyote.
5. Hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai au uhalifu.
6. Kiwango cha chini cha sifa za kitaaluma kitakuwa ngazi ya diploma
7. Kikomo cha umri wa mwombaji kitakuwa miaka 70.
8. Atapaswa kuwasilisha nyaraka zote muhimu kama ilivyoelezwa katika kifungu kidogo cha 2.1 katika kanuni za uchaguzi ya TCCIA.
9. Kiongozi yeyote akichaguliwa atalazimika kusaini Kanuni za maadili za TCCIA.
10. Mgomba anayewania nafasi ya uongozi atahitajika kulipa ada ya maombi isiyoweza kurejeshwa (non refundable) ya kiasi cha Tshs. 200,000 kupitia

Jina la Benki: CRDB

Namba ya Akaunti: 01J 1043816400

Jina la Akaunti: TCCIA/SIDA Winding Up

Fomu zote ziwasilishwe kwa njia ya mtandao kupitia hq@tccia.com au nakala ngumu zitumwe TCCIA Makao Makuu kabla ya saa kumi na moja kamili (11:00) jioni tarehe 24 Octoba 2023.

Imetolewa leo tarehe 6 Octoba 2023.

Wenu,

Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).



Mwanahamisi Husein,
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji.

TANZANIA CHAMBER OF COMMERCE
INDUSTRY AND AGRICULTURE
P.O. Box 9713 DARES SALAAM